**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA

**WAKALA YA SERIKALI MTANDAO**

Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano, Ghorofa 3 S.L.P. 2833, 40404Dodoma,
Simu: +255222129868Barua pepe: info@ega.go.tz, CEO Barua Pepe: ceo@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## MATUMIZI YA TEHAMA KATIKA KUBORESHA UTENDAJI KAZI SERIKALINI

Wakala ya Serikali Mtandao imebuni, imesanifu na imetengeneza mfumo shirikishi wa **Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS).** Mfumo huu unaunganisha shughuli mbalimbali za Taasisi kuwa katika mfumo mmoja unaowezesha usimamizi, ufuatiliaji, ukaguzi na tathimini ya utekelezaji wa shughuli zote za Taasisi kwa ufanisi.

Akifafanua kuhusu mfumo huu, Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt, Jabiri Bakari amesema, "Tumeamua kutumia utajiri wa utaalamu wetu wa kidigitali kutengeneza Mfumo huu (ERMS) ambao ni dirisha moja linalounganisha shughuli zote ndani ya Taasisi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma."

ERMS ina moduli kumi na nane (18) zinazounganisha shughuli mbalimbali za utendaji kazi zinazotegemeana na kuwezesha kubadilishana taarifa miongoni mwa idara/vitengo na kusimamia raslimali kama vile watu, fedha na vitendea kazi. Mfumo huu pia unawezesha ushughulikiaji wa miamala kutoka idara moja hadi nyingine kama vile ankra za bidhaa na huduma, mapato na matumizi, ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli kulingana na mipango na bajeti, usimamizi wa majukumu ya watumishi, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi, utekelezaji wa shughuli za ununuzi na utayarishaji wa taarifa mbalimbali za utendaji. Amesema Dkt. Bakari.

Aidha, Dkt. Bakari alieleza kuwa mfumo huu una "dashboard" ambayo inawawezesha Maafisa Masuuli na watumiaji wengine wa mfumo kupata taarifa mbalimbali kulingana na mahitaji yao. Taarifa hizo zinaweza kuwa za fedha, vifungu vya bajeti na bakaa ya fedha, hali ya matumizi ya fedha, taarifa zinazosaidia katika upimaji wa utendaji wa watumishi, na hivyo kusaidia katika utoaji wa maamuzi sahihi.

ERMS pia inaweza kuunganishwa na kubadilishana taarifa na mifumo mingine Mikuu ya Serikali kama vile Mfumo mkuu wa uhasibu, Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu (HCMIS), Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG), Mfumo wa Barua pepe Serikalini (GMS), Mfumo wa Ofisi Mtandao na kadhalika. Aidha Moduli za Mfumo huu zinaweza kuongezwa au kupunguzwa bila kuathiri utendaji kazi wa moduli nyingine au mfumo kwa ujumla.

Akielezea mifumo mingine iliyotengenezwa na Wakala katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini, Dkt. Bakari ametaja mifumo hiyo kuwa ni pamoja na kuhuishwa kwa iliyokuwa

Tovuti ya Serikali na kuwa Tovuti Kuu ya Serikali www.tanzania.go.tz, inayosimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambayo ni dirisha moja la kutolea taarifa na huduma za Serikali kwa wananchi; Tovuti Kuu ya Ajira http://portal.ajira.go.tz, inayosimamiwa na Sekretariati ya Ajira; Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS) unaotumiwa na Taasisi za umma 402 zikiwemo ofisi za Ubalozi nje ya nchi, kwa ajili ya kubadilishana taarifa Serikalini.

Mifumo mingine ni pamoja na Ofisi Mtandao, ambao unawezesha na kurahisisha shughuli za utawala za kila siku hususani mzunguko wa majalada na nyaraka ndani na miongoni mwa Taasisi za umma, Taasisi za umma 52 zinatumia mfumo huu mpaka sasa; Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi (mGov) (http://mgov.ega.go.tz), unaopatikana kupitia namba ***152*00#**, ambao ni dirisha moja la huduma Serikali kupitia za simu za mkononi. mGov imeunganishwa na watoa huduma wote wakubwa wa simu za mkononi na unatumiwa na Taasisi za umma 147 mpaka sasa.

Mfumo mwingine ambao umetengenezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ambao ndio wasimamizi wakuu wa Mfumo huu ni Mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG). Mfumo huu unalenga kuongeza udhibiti katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato Serikalini. Mfumo huu unatumiwa na Taasisi za umma 385, watoa huduma za malipo 17 ambao ni Benki Kubwa 12 (NMB, STANBIC, NBC, CRDB, EXIM, TIB, BOT, ECOBANK, PBZ, DCB, DTB na TPB), Mifumo ya Fedha ya Simu za Mkononi 5 (Tpesa, TigoPesa HaloPesa, Mpesa na Airtel Money), mpaka sasa. Alieleza Dkt. Bakari.

Aidha, kuna mfumo wa e-Vibali (https://safari.gov.go.tz), ambao unatumiwana na taasisi 389 katika kuomba na kupata vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa safari za kikazi na binafsi kwa watumishi wa umma. Aidha, kuna mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Miradi ya TEHAMA Serikalini (GIP) ambao unatumiwa na taasisi takribani 77; Mfumo wa Huduma kwa Mteja unaopatikana kupitia (http://helpdesk.ega.go.tz) au kupitia baruapepe egov.helpdesk@ega.g.tz unaotumika kutoa huduma na msaada wa kiufundi kwa huduma zinazotolewa na Wakala. Taasisi 315 zinatumia Mfumo huu na jumla ya matatizo 5,187 yanayohusu TEHAMA yameshughulikiwa; na Mfumo wa Usimamizi wa Tiketi na Mizigo kielektroni (e-ticket and Cargo System) unaotumiwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Pamoja na hayo, Dkt. Bakari amezishauri Taasisi za umma kuendelea kutumia vizuri TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi Serikalini na utoaji huduma kwa umma kwa kuzingatia miongozo na viwango vya Serikali Mtandao vinavyopatikana katika tovuti ya Wakala https://www.ega.go.tz/standards. "Kinachohitajika ni ujuzi stahiki na kujiamini ili kupata matokeo bora na ya haraka. Aidha Wakala itaendelea kutoa ushauri na msaada wa kiufundi katika utekelezaji wa Serikali mtandao kwa taasisi za umma."

Imetolewa na
Wakala ya Serikali Mtandao
Aprili 29, 2019